BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 19 Mei, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

199. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

(a) Kuna kauli mbiu zipi ambazo zinatumika katika suala zima la uhifadhi wa mazingira kwa usalama wa maisha ya binadamu.

(b) Kwa kiasi gani kauli mbiu hizo zinaleta tija na mabadiliko chanya.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

215. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kiasi gani Tume ya Haki za Binadamu inasimamia ipasavyo suala zima la kupokea malalamiko ya wananchi na kuyafanyia kazi ipasavyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

10. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kuna haja gani ya kuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha iliyoanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini utendaji kazi wake bado unaendelea kulalamikiwa siku hadi siku.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

132. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kumekuwa na hali mbaya na matumizi yasiyo sahihi katika Nyumba za Maendeleo Mijini na Vijijini Unguja na Pemba pamoja na uchakavu wa nyumba hizo.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hili.

(b) Je, Serikali ina mpango gani juu ya matengenezo ya nyumba hizi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

240. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tatizo la umeme mdogo linasababisha baadhi ya huduma kushindwa kutolewa kwa ufanisi hususani katika mashine ya vituo vya maji.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi tatizo hilo liliopo katika kituo cha maji cha Mtule na Kitogani.

(b) Je, ni lini tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa maeneo hayo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

21. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sensa ya miti (wood biomass survey) ni nyenzo muhimu ya kufahamu mabadiliko ya uoto wa asili, wingi wa misitu tuliyonayo na idadi ya mikarafuu. Hadi sasa, Zanzibar haijafanya sensa hii ya miti ambayo ni muhimu ili kubaini miti iliyoko katika hatari ya kutoweka na kuweka mkazo katika kuilinda.

(a) Je, ni ipi tathmini ya sensa ya miti iliyopo hivi sasa kwa uoto wa asili, misitu na mikarafuu.

(b) Je, ni upi muongozo wa kitaifa na kimataifa katika kufanyika sensa ya miti katika nchi.

(c) Je, ni changamoto zipi ambazo Serikali imekumbana nazo hadi kushindwa kufanya sensa hii ya miti.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

181. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Mambo gani makubwa ya kimaendeleo ya kujivunia katika suala zima la uchumi wa buluu ikiwa na mchango mkubwa kutoka kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**19 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**